

Kukumbuka pamoja na Bibi



Kwa nini Mari amekuwa hana subira na Bibi?



Na Jane McBride
(Imetokana na hadithi ya kweli)

Mari alinuna. Bibi alikuwa ana-simulia hadithi ile ile. Tena. Bibi alikuja kuishi pamoja na familia ya Mari miezi kadhaa ili-yopita. Mari alimpenda, lakini kuwa karibu na Bibi wakati mwingine kulichosha. Alisimulia hadithi ile ile tena na tena. Wakati mwingine alianza tena kabla hata hajamaliza kusimulia hadithi.

Mari alishusha pumzi. "Bibi" Mari alisema, "ume-kwishanisimulia hadithi hiyo."

Bibi alitazama chini. "Tayari?"

"Ndio," Mari alisema. "Umenisimulia dakika chache tu zilizopita."

"Sikumbuki," Bibi ali-sema. Bibi alionekana kuhuzunika na kuchanganyikiwa. Kisha alisimama na kurudi chumbani kwake.

Mari alihuzunika kwamba alikuwa ame-mkasirisha Bibi. Tangu kufariki kwa Babu, Bibi amekuwa mwenye kus-hau sana na sana zaidi. Wakati mmoja aliacha jiko liki-wa linawaka, na likaanzisha moto jikoni kwake. Huo ni wakati ambao Mama na Baba walimleta Bibi kuishi pamoja nao.

Mari alimpata Baba jikoni. "Ninampenda Bibi sana, lakini ninachoka kusikiliza hadithi zile zile. Kwa nini hakumbuki kwamba yeye alikuwa tayari ameniambia hadithi hiyo kari-bia mara milioni hamsini?"

Baba akatabasamu. "Nina hakika si mara *milioni* hamsini. Lakini najua ni vigumu. Bibi yako ana maradhi katika akili yake ambayo yanamfanya asahau vitu. Hadithi zake ni njia yake ya kujaribu kukumbuka yeye ni nani."

Mari aliinamisha kichwa chake. Kwa nini hakuwa na subira sana na Bibi yake? Bibi daima alikuwa anamtendea kwa upendo. Alimwita "Mari wangu." Mari alifikiria kuhu-su wakati alipomsaidia Bibi kupanda maua na kung'oa magugu bustanini.

Mari aligonga mlango wa Bibi.



"Ingia ndani," Bibi alisema.

Mari alifungua mla-ngo. Bibi alikuwa ame-keti kwenye kiti na maandiko yaliyofungu-liwa kwenye paja lake.

"Bibi, tafadhali una-weza kuniambia jinsi wewe na Babu mlijiunga na Kanisa?" Mari aliomba. Bibi akatazama juu. "Una-taka kusikia kuhusu Babu pamoja na mimi?" aliuliza kwa sauti ya tumaini.

Mari aliketi karibu na Bibi. "Ndio. Nataka kusikia kila kitu." Mari aliutwaa mkono wa Bibi yake. "Wewe ni maalum kwangu, Bibi. Wewe daima utakuwa hivyo."

Bibi alitabasamu, akakaa kwenye kiti cha-ke, na kuanza kusimulia hadithi.

Mari alikuwa amesikia hadithi hii mara nyingi, lakini wakati huu, hakuudhika au hakukosa subira. Badala yake, alihisi upendo na mshangao. Aliuja Bibi na Babu walikuwa wamefanya dhabihu sana walipo-jiunga na Kanisa huko Ujeruman. Babu na Bibi yake walihamia mbali kutoka nyumbani kwao ili waweze kuishi karibu na waumini wengine wa Kanisa.

Bibi alimaliza hadithi na kutabasamu. "Wewe ni msichana mzuri, Mari wangu."

Mari alimkumbatia Bibi yake. "Asante, Bibi. Ninakupenda." ●

Hadithi hii ilitokea huko Marekani.